na mchira wa tala.” ¹⁵ Phahi mfalume waapaza atu hinyo, mana Mwenyezi Mlungu walonda ikale hivyo ili atimize nenore ariromuambira Jeroboamu mwana wa Nebati, kutsupira Ahija kula Shilo.

¹⁶ Phahi, atu osi a Iziraeli ariphoona kukala mfalume kaaphundza, amuambira: “Huna mtalo wani swino kpwa Daudi? Tahuna urisi wowosi kpwa mwana wa Jese. Uyani kpweni, mwimwi Aiziraeli! Kamanyirire mwenye nyumbayo, uwe Daudi.” Phahi Aiziraeli achiuya chila mutu kpwakpwe. ¹⁷ Ela Rehoboamu waenderera kuatawala Aiziraeli okala kpwenye midzi ya Juda bahi. ¹⁸ Chisha mfalume Rehoboamu wamuhuma Hadoramu ambaye kala ni muimirizi wa kazi za shokowa aphiye kpwa Aiziraeli a vurini, ela nyo achimpiga mawe hadi achifwa. Mfalume Rehoboamu wapanda mairo kpwenye garire ra kuvwehwa ni farasi achichimbirira Jerusalemu. ¹⁹ Phahi hangu phapho Aiziraeli a vurini arema kutawalwa ni mbari ya Daudi hadi rero.

11

Rehoboamu anaimarisha ufalumewe (1 Afalume 12:21–24)

¹ Rehoboamu ariphofika Jerusalemu wakusanya atu elufu gana mwenga na mirongo minane, masujaa a viha kula kpwa mbari ya Juda na mbari ya Benjamini, ili apigane na Aiziraeli a vurini na auyize ufalume wosi ukale tsiniye. ² Ela Mwenyezi Mlungu achigomba na Shemaya

mutu wa Mlungu achimuamba, ³ “Muambire Rehoboamu mwana wa Selemani, mfalume wa Juda na Aiziraeli osi ario Juda na Benjamini na atu anjina, ⁴ kukala mimi Mwenyezi Mlungu naamba hivi, ‘Musiphiye, wala msipigane na ndugu zenu. Chila mutu auye kpwakpwe kaya, mana higo chigohendeka ni mpango wangu.’ ” Phahi nyo arilunga neno ra Mwenyezi Mlungu na achiuya wala taayaphiya kpwendapigana na Jeroboamu.

⁵ Naye Rehoboamu wasagala Jerusalemu, achidzenga midzi yenye ngome hiko Juda. ⁶ Wadzenga Bethlehemu, Etamu, Tekoa, ⁷ Bethi-Suri, Soko, Adulamu, ⁸ Gathi, Maresha, Zifu, ⁹ Adoraimu, Lakishi, Azeka, ¹⁰ Zora, Aijaloni na Heburoni, midzi yenye ngome iriyo hiko Juda na Benjamini. ¹¹ Hizo ngome waziika imara nazo zaimirirwa ni akulu a jeshi na kala zina vyumba vya kuikira chakurya, mafuha ga zaituni na uchi wa zabibu. ¹² Na kpwenye chila mudzi watiya ngao na mafumo, ili ukale na nguvu nyinji sana. Hivyo Juda na Benjamini ichikala tsini ya utawalawe.

*Alavyadzi-sadaka na Alawi
anaunga mkpwono Rehoboamu*

¹³ Na alavyadzi-sadaka na Alawi osi arioishi Iziraeli kosi amuunga mkpwono Rehoboamu. ¹⁴ Hinyo Alawi aricha makalo gao na midzi yao ya marisa hiko Iziraeli na achiphiya Jerusalemu na midzi yanjina ya Juda, kpwa mana Jeroboamu na anae waatsupha, ili asimuhendere Mwenyezi Mlungu huduma ya ulavyadzi-sadaka.

15 Jeroboamu wadzitsamburira alavyadzie-sadaka mwenye ahumike hiko mizukani mwatu mwa dzulu, mwatu mokala na majine na vira vizuka vya ndama arivyovitengeza. 16 Na kula mbari zosi za Iziraeli, atu ariolonda kuabudu Mwenyezi Mlungu chikpweli-kpweli kala achialunga alavyadzi-sadaka hiko Jerusalemu, ili kumlavira sadaka Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare ao. 17 Chihivyo ufalume wa Juda waimarishwa kpwa miaka mihahu naye Rehoboamu mwana wa Selemani achitiywa nguvu, kpwa mana muda hinyo wa miaka mihahu, atu aenderera kulunga dza siku za Daudi na Selemani. 18 Rehoboamu walóla Mahalathi mwana mchetu wa Jerimothi wa chivyazi cha Daudi. Nine kala ni Abihaili mwana mchetu wa Eliabu, mwana wa Jese.

Rehoboamu na atu a nyumbaye

19 Rehoboamu na Mahalathi avyala ana ahahu a chilume: Jeushi, Shemaria na Zahamu. 20 Chisha bada ya hiye achilóla Maaka, mwana mchetu wa Abusalomu. Naye wamvyarira Abija, Atai, Ziza na Shelomithi. 21 Rehoboamu wammendza Maaka mwana mchetu wa Abusalomu kutsupa ahee osi na anachetue osi, mana kala walóla achetu mrongo mmwenga na anane na anachetu mirongo sita. Naye wavyarirwa ana alume mirongo miiri na anane na achetu mirongo sita. 22 Rehoboamu wahenda Abija mwana wa Maaka akale mkpwulu kahi ya nduguze, kpwa mana kala analonda

amtawaze akale mfalume. ²³ Rehoboamu wahumira achili, achiatawanya anae a chilume kpwenye midzi yosi ya Juda na Benjamini yenye ngome. Waaphirikira chakurya chinji na achialoza achetu anji.

12

Amisiri anavamia Juda (1 Afalume 14:25–28)

¹ Mara tu Rehoboamu ariphoimarisha ufalumewe na kuphaha nguvu, iye phamwenga na Aiziraeli osi aricha kulunga shariya ya Mwenyezi Mlungu. ² Mwaka wa tsano wa utawala wa mfalume Rehoboamu, Shishaki mfalume wa Misiri washambuliya Jerusalemu, mana Aiziraeli kala sio aaminifu kpwa Mwenyezi Mlungu. ³ Shishaki wakpwendavamia na magari ga kuvwehwa ni farasi elufu mwenga na magana mairi na anajeshi akuhumira farasi elufu mirongo sita na anajeshi a kunyendeka na magulu asiolangika. Nao kala ni Alibiya, Asukii na Akushi ariokpwedza nao kula Misiri. ⁴ Wateka midzi yosi ya Juda yokala na ngome, achedza hadi Jerusalemu. ⁵ Ndipho nabii Shemaya achedza kpwa Rehoboamu na kpwa akulu a Juda ambao kala akakusanyika Jerusalemu kpwa kumuogopha Shishaki, achiambira, “Mwenyezi Mlungu anaamba hivi, ‘Mwimwi mwaniricha nami nkakurichani mikononi mwa Shishaki.’” ⁶ Ndipho akulu a Iziraeli na mfalume asononeka kpwa sababu ya makosa gao achiamba, “Mwenyezi Mlungu ndiye mwenye haki.” ⁷ Naye

Mwenyezi Mlungu ariphoona kukala hinyo atu akasononekera makosa gao, Mwenyezi Mlungu wagomba kutsupira Shemaya kuamba, “Akalalama sindaabananga ela nindaativya wala usiru wangu sindaumwagira Jerusalemu kutsupira mkpwono wa Shishaki. ⁸ Ela phahi andamuhumikira ili aphahe kumanya tafwauti kahi ya kunihumikira mimi na kuhumikira afalume a dunia.”

⁹ Phahi Shishaki mfalume wa Misiri waambuka hadi Jerusalemu, achihala hazina zosi za nyumba ya Mwenyezi Mlungu na hazina za nyumba ya mfalume. Piya achihala ngao za zahabu zotengezwa ni mfalume Selemani.

¹⁰ Naye mfalume Rehoboamu achitengeza ngao za shaba badalaye na achizipha akulu a arindzi ariorinda mryango wa nyumba ya mfalume. ¹¹ Chila mfalume ariphoinjira nyumbani mwa Mwenyezi Mlungu, arindzi a ryango azihala, na badaye aziuyiza chumba cha arindzi a ryango. ¹² Naye Rehoboamu aripholalama, usiru wa Mwenyezi Mlungu wauka, kayam’bananga tsetsetse. Chisha mambo manono gaoneka hiko Juda.

*Utawala wa Rehoboamu kpwa ufupi
(1 Afalume 14:21,29–31)*

¹³ Phahi mfalume Rehoboamu wadziimarisha hiko Jerusalemu na achitawala. Naye kala ana miaka mirongo mine na mmwenga ariphoandza kutawala. Na watawala miaka mrongo mmwenga na sabaa hiko Jerusalemu,

mudzi uriotsambulwa ni Mwenyezi Mlungu kahi za mbari zosi za Iziraeli, ili aabudiwe hiko. Nine kala anaihwa Naama, wa kabila ra Aamoni. ¹⁴ Naye wahenda mai, kpwa kukala moyowe kayawelegeza kumuendza Mwenyezi Mlungu.

¹⁵ Phahi mambo ga Rehoboamu, hangu mwandzo hata mwisho, gaandikpwa kpwenye chitabu cha kumbukumbu cha nabii Shemaya na kumbukumbu za Ido muonadzi. Kpwakala na viha vya vivyo kpwa vivyo kahi ya Rehoboamu na Jeroboamu. ¹⁶ Rehoboamu wafwa, achizikpwa kpwenye Mudzi wa Daudi na mwanawe Abija achitawala badalaye.

13

Utawala wa Abija hiko Juda (1 Afalume 15:1-8)

¹ Abija waandza kutawala Juda mwaka wa kumi na nane wa utawala wa Jeroboamu.

² Watawala miaka mihahu hiko Jerusalemu. Nine kala aihwa Maaka mwana mchetu wa Urieli kula Gibeya.

Kpwakala na viha kahi ya Abija na Jeroboamu.

³ Abija waphiya vihani na jeshi ra masujaa a viha elufu magana mane. Jeroboamu naye achedza na akpwe elufu magana manane, atu a nguma akumanya viha.

⁴ Phahi Abija waima dzulu ya chidzango Semaraimu chiricho myangoni mwa Efuraimu achiamba, “We Jeroboamu na Aiziraeli mosi niphundzani!

⁵ Dze, mwino tammanya kukala Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa Iziraeli

wamupha ufalume Daudi na chivyaziche hata kare na kare kpwa chilagane chisichovundzika?*

⁶ Ela Jeroboamu mwana wa Nebati, mtumishi wa Selemani wamuasi mfalumewe. ⁷ Chisha atu ayi asinyofwaha chitu, adziunga phamwenga naye, achimpinga Rehoboamu mwana wa Selemani ariphokala dang'a ra mwana ambapho kangeweza kushindana nao. ⁸ Na vino sambi munaona mundaupinga ufalume wa Mwenyezi Mlungu unaolongozwa ni mbari ya Daudi, kpwa kukala mu ndulu ya atu namwi muna vizuka vya ana ng'ombe a zahabu muriotengezerwa ni Jeroboamu? ⁹ Avi mwino mwaazoresa alavyadzi-sadaka a Mwenyezi Mlungu, ana a Aruni na Alawi, mchidzitsamburira alavyadzi-sadaka dza ahendavyo atu a tsi zanjina? Hata mutu yeyesi edzaye na mwana ng'ombe au maturume sabaa kpwa alavye sadaka anaweza kukala mlavyadzi-sadaka wa iyo isiyokala milungu.

¹⁰ “Ela swino, Mwenyezi Mlungu ndiye Mlungu wehu naye tahudzangbwemricha. Swino huna alavyadzi-sadaka, ana a Aruni, ambao anamuhumikira Mwenyezi Mlungu na anaterywa ni Alawi. ¹¹ Nao ligundzu na dziloni anamlavira Mwenyezi Mlungu sadaka za kuochwa na kufukiza uvumba wa kunukato. Mikahe mitakatifu nkuyiika dzulu ya meza ya zahabu swafi. Piya aho nkuasa taa zirizo kpwenye chinara cha zahabu chila dziloni, kpwa mana swino hunalunga malagizo ga Mwenyezi Mlungu, Mlungu wehu, ela mwino mwamricha. ¹² Lolani, Mlungu a

* **13:5** 13:5 Chilagane chisichovundzika hipha Chieburania chinaamba Chilagane cha munyu.

phamwenga naswi anahutanguliya. Alavyadzie-sadaka na tarumbeta zao za viha andazipiga ili huandze viha namwi. Mwino ana a Iziraeli richani kupigana na Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare enu mana tamundaweza kumtura.”

¹³ Ela Abija ariphokala anagomba hivyo, Jeroboamu wahuma seemu ya jeshire chisiri-siri kuazangira kpwa nyuma. Phahi baazi ya ana-jeshi a Jeroboamu achikala mbere za Juda na hinyo aoteao achikala nyuma za atu a Juda.

¹⁴ Na atu a Juda aripholola nyuma, ke, kala anavamiwa mbere na nyuma zao! Phahi amririra Mwenyezi Mlungu, alavyadzi-sadaka achipiga tarumbeta zao ¹⁵ na jeshi ra Juda richipiga zumo ra viha. Jeshi ra Juda ririphopiga hiro zumo ra viha, Mlungu wamturya Jeroboamu na jeshi rosi ra Iziraeli mbere za Abija na jeshi ra Juda. ¹⁶ Hiro jeshi ra Iziraeli rachimbira mbere za jeshi ra Juda naye Mlungu achiatiya Iziraeli mikononi mwa Juda. ¹⁷ Phahi Abija na jeshire waapiga sana hata achiolaga apiganadzi hodari a Iziraeli, elufu magana matsano. ¹⁸ Hivyo ndivyo atu a Iziraeli arivyoshindwa siku hizo. Jeshi ra Juda ashinda kpwa kukala amkuluphira Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare ao.

¹⁹ Naye Abija wamzoresa Jeroboamu hata achimfuta mudzi wa Betheli na malaloge, mudzi wa Jeshana na malaloge na mudzi wa Efuroni na malaloge. ²⁰ Wala Jeroboamu kayakala na nguvu tsona za kupigana viha siku za utawala wa Abija. Mwishirowe Mwenyezi Mlungu wampiga naye achifwa. ²¹ Ela Abija wazidi kukala na nguvu za viha. Naye walóla achetu kumi na a ne na

achivyala ana alume mironko miiri na airi na ana achetu kumi na sita. ²² Na mambo ganjina ga Abija, arigohenda na arigogomba, gaandikpwa kpwenye chitabu cha kumbukumbu cha nabii Ido.

14

Mfalume Asa wa Juda

¹ Phahi Abija wafwa na achizikpwa kpwenye mudzi wa Daudi. Mwanawe Asa watawala badalaye. Siku za utawala wa Asa, tsi yakala na amani kpwa miaka kumi. ² Asa wahenda mambo manono na ga haki mbere za Mwenyezi Mlungu, Mlunguwe. ³ Iye wausa mwatu mwa kulavira sadaka za milungu ya chijeni na mwatu mwa dzulu mwa ibada na kuvundza sanamu za nguzo za mawe. Nguzo za Ashera nazo wazivundza-vundza. ⁴ Naye waamuru atu a Juda aendze Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare aho na alunge shariyaze na amurize. ⁵ Chisha wausa kula kpwa midzi yosi ya Juda mwatu mwa dzulu mwa ibada na himo mwatu mwa kufukizira uvumba. Ndipho ufalume wa Asa uchikala na amani. ⁶ Wadzenga midzi yenye ngome hiko Juda kpwa kukala tsi yakala na amani. Miaka iyo kayakala na viha mana Mwenyezi Mlungu wamupha amani. ⁷ Chisha achiambira atu a Juda, “Midzi hino huidzengeni na huizungulusire kuta na minara, maryango na magbwama. Hino tsi bado ni yehu mana hukamlunga Mwenyezi Mlungu, Mlungu wehu. Hukaendza Mlungu naye akahupha amani chila uphande.” Nao adzenga na achiongokerwa.

⁸ Asa hiko Juda kala ana jeshi ra atu elufu magana mahahu okala na ngao na mafumo. Na hiko Benjamini wakala na atu elufu magana mairi na mirongo minane enye ngao, maha na mivi. Hinyo osi kala ni masujaa ga viha.

⁹ Wakati mmwenga, Zera kula Kushi washambuliya Juda na jeshi ra atu milioni mwenga na magari magana mahahu ga kuvwehwa ni farasi, achedza hadi Maresha. ¹⁰ Phahi Asa wakpwendapigana naye na achipanga viha Dete ra Zefatha hiko Maresha.

¹¹ Asa wamririra Mwenyezi Mlungu, Mlunguwe achiamba, “Mwenyezi Mlungu, taphana wanjina dza uwe awezaye kuterya kahi ya mwenye mkpwotse na mnyonje. Ee Mwenyezi Mlungu, huterye kpwa mana swino hunakukuluphira uwe. Naswi hukedzapigana na jeshi hiri kulu kpwa dzinaro. Ee Mwenyezi Mlungu, uwe ndiwe Mlungu wehu, usiriche mwanadamu akakuturya.”

¹² Hipo, Mwenyezi Mlungu waapiga Akushi mbere za Asa na jeshi ra Juda, nao Akushi achichimbira. ¹³ Asa na atu okala phamwenga naye achiazoresa hata Gerari. Phahi Akushi aphukusika taphayasala hata mmwenga. Mana osi tsetsetse aangamizwa ni Mwenyezi Mlungu na jeshire. Atu a Juda ahala zewe vitu vinji sana.

¹⁴ Alafu apiga midzi yosi yokala kanda-kanda ya Gerari mana enyezi a midzi iyo kala akainjirwa ni wuoga wa Mwenyezi Mlungu. Midzi yosi aihala zewe mana kala ina vitu vinji sana.

¹⁵ Piya ashambuliya kambi za afugadzi, achihala

mang'ondzi manji na ngamia, ndipho achiuya Jerusalemu.

15

Asa anavundza-vundza vizuka hiko Juda

¹ Chisha Roho wa Mwenyezi Mlungu wamwedzera Azaria mwana wa Odedi, ² naye achituluka ili akakutane na Asa, achimuambira, “Uwe Asa na atu a Juda na atu a Benjamini mosi niphundzani, Mwenyezi Mlungu a phamwenga namwi napho mundakala phamwenga naye. Mchimuendza Mwenyezi Mlungu mundamphaha, ela muchimuricha naye andakurichani. ³ Kpwa siku nyinji, atu a Iziraeli kala taana Mlungu wa kpweli, wala mlavyadzi-sadaka wa kuafundza, wala shariya. ⁴ Ela napho akaphahwa ni mashaka achimuuyira Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa Iziraeli na amuendzapho, nkumphaha. ⁵ Siku hizo kala takuna amani kpwa atulukaye wala ainjiraye mana wasiwasi mkpwulu wamfika chila ariyesagala tsi hizo. ⁶ Taifa mwenga raangamizwa ni taifa ranjina, na mudzi uchiangamizwa ni mudzi wanjina, kpwa kukala Mlungu waarehera mashaka ga chila aina. ⁷ Ela mwimwi dinani chilume! Msivundzike moyo, mana mundatuzwa kpwa kazi yenu.”

⁸ Naye Asa ariphosikira maneno higo, yani hinyo unabii wa Azaria mwana wa Odedi, wamenya nguvu naye achiusa vizuka vyosi vya kut-sukiza kula kpwa tsi yosi ya Juda na Benjamini. Na piya kula kpwa midzi yosi yokala akaiteka ya

tsi ya myango ya Efuraimu. Chisha achitengeza uphya phatu pha kulavira sadaka pha Mwenyezi Mlungu phokala mbere ya baraza ya Nyumba ya kuvoya Mlungu. ⁹ Asa waakusanya atu osi a Juda na Benjamini na hara ajeni ariola Efuraimu na Manase na Simioni ambao kala anasagala nao, kpwa mana atu anji atuluka Iziraeli ya vurini achimlunga ariphoona kukala Mwenyezi Mlungu a phamwenga naye.

¹⁰ Phahi akusanyika hiko Jerusalemu mwezi wa hahu, mwaka wa kumi na tsano wa utawala wa Asa. ¹¹ Siku hiyo, amlavira Mwenyezi Mlungu sadaka ndzau magana sabaa, mang'ondzi na mbuzi elufu sabaa kula kpwa zewe arizozihala vihani. ¹² Nao aika chilagane cha kukala andaenda Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare aho na mioyo yao yosi na roho zao zosi. ¹³ Chisha achikubaliana kukala yeyesi ambaye kandamuenda Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa Iziraeli andaolagbwa, akale mvyere au mdide, akale mlume au mchetu. ¹⁴ Aapa kpwa Mwenyezi Mlungu na raka ra dzulu na kukota kululu, kupiga tarumbeta na kupiga magunda. ¹⁵ Atu osi a Juda ahererwa kpwa kuapa chirapho hicho, kpwa kukala aapa kpwa mioyo yao yosi. Nao amuenda Mwenyezi Mlungu kpwa kumenda kpwao enye na achimphaha. Mwenyezi Mlungu waahenda akale na amani na aviha aho a chila uphande.

¹⁶ Mfalume Asa wamfuta cheo cha umalikia wawaye yeihwa Maaka kpwa kukala watengeza chizuka cha Ashera ambacho kala ni tsukizo. Iye wachivundza-vundza na achichiocha kpwenye

Dete ra Kidironi. ¹⁷ Dzagbwe kayabananga mwatu mwa dzulu mwa kuabudu milungu kahi za Iziraeli, Asa kala ni muaminifu kpwa Mwenyezi Mlungu maishage gosi. ¹⁸ Naye wareha nyumbani mwa Mlungu miyo ya feza na ya zahabu yotengbwa kpwa ajili ya Mlungu ni ise na yoitenga ye mwenye. ¹⁹ Na wala takuyakala na viha tsona wakati wa utawala wa Asa hadi mwakawe wa mirongo mihahu na tsano wa kutawala.

16

Mfalume Baasha wa Iziraeli anavamia Juda

(1 Afalume 15:16–22)

¹ Mwaka wa mirongo mihahu na sita wa utawala wa Asa, Baasha mfalume wa Iziraeli waambuka kpendashambuliya tsi ya Juda, na achidzenga ngome ko mudzi wa Rama, ili aphahe kuzuwiya mutu yeyesi kutuluka wala kuinjira tsi ya Asa, mfalume wa Juda.

² Ndipho Asa achituluzza feza na zahabu kula kpwa hazina ya Nyumba ya Mwenyezi Mlungu na kula kpwa nyumba ya mfalume, achimphirikira Beni-Hadadi mfalume wa Shamu, yesagala Damasikasi, achimuamba, ³ “Nahuike mapatano ga ushirikiano kahi yangu na uwe dza vira baba na sowe arivyohenda. Lola, nkalagiza ureherwe feza na zahabu. Phahi phiya ukavundze mapatanogo na Baasha, mfalume wa Iziraeli, ili ariche kunishambuliya.” ⁴ Naye Beni-Hadadi wamphundza mfalume Asa, achihuma akulu a jeshi kpendapiga midzi ya Iziraeli.

Wakpwendaturya midzi ya Ijoni, Dani, Abeli-Maimu na midzi yosi ya kuikira vitu vya Nafutali. ⁵ Mfalume Baasha ariphophaha habari, waricha kudzenga mudzi wa Rama, na achiyimisa yo kaziye.

⁶ Ndipho mfalume Asa achiareha atu osi a Juda, nao achitsamiza mawe ga Rama, na mbaoze, vitu ambavyo Baasha kala anadzengera. Mfalume Asa achivihumira kudzengera mudzi wa Geba na mudzi wa Mizipa.

Nabii Hanani anamuamula Asa

⁷ Wakati hinyo muonadzi Hanani wakpwedza kpwa Asa mfalume wa Juda achimuamba, “Kpwa kukala ukamkuluphira mfalume wa Shamu kuriko Mwenyezi Mlungu, Mlungu, nawe kundaweza kurishinda tsona jeshi ra mfalume wa Shamu. ⁸ Kpwani nyo Akushi na Alibiya kala siro jeshi kulu sana renye magari manji ga kuvwehwa ni farasi na apherikie? Ela Mwenyezi Mlungu ye waatiya mwako mkp-wononi kpwa vira uwe wamkuluphira. ⁹ Kpwa mana matso ga Mwenyezi Mlungu nkulola chila phatu kosi duniani, ili aatiye nguvu hara anaomkuluphira iye chikamilifu. Ukahenda dzambo ra chizuzu nawe kuandzira sambu undakala na viha.” ¹⁰ Phahi Asa wareyezwa ni hiye muonadzi ariphosikira maneno higo, achimtiya jela kpwa mana akamtsukiza. Wakati hinyo piya, Asa waandza kuaonera atu anjina.

Asa anafwa
(1 Afalume 15:23–24)

¹¹ Mahendo ganjina ga Asa, kula mwandzo hadi mwisho, gaandikpwa kpwenye Chitabu cha Afalume a Juda na a Iziraeli. ¹² Iriphofika mwaka wa mirongo mihahu na tisiya wa utawalawe, Asa wagbwirwa ni ukongo wa magulu. Nyo ukongowe wamzidiya sana, ela hata ariphozidiywa kayamuendza Mwenyezi Mlungu badalaye waendza msada kpwa aganga. ¹³ Phahi Asa wafwa mwaka wa mirongo mine na mwenga wa utawalawe. ¹⁴ Achizikpwa kpwenye mbira yokala akadzitsongera, ko Mudzi wa Daudi. Achimlaza dzulu ya chitanda chokala chikaodzazwa chila aina ya vilungo virivyotayarishwa ni atu amanyao kutengeza manukato. Chisha achikuta moho mkpwulu sana kpwa ishimaye.

17

Jehoshafati mfalume wa Juda

¹ Jehoshafati mwana wa Asa watawala badala ya ise naye wadzitiya nguvu ili aaturye Aiziraeli a vurini. ² Waika majeshi kpwenye midzi yosi ya Juda yenye kuta. Waika asikari arindzi hiko tsi ya Juda na ndani ya midzi ya Efuraimu yokala ise kala akaiteka.

³ Mwenyezi Mlungu wakala phamwenga na Jehoshafati mana katika sikuze za mwandzo za kutawala walunga njira za mkarewe Daudi wala kayaabudu vizuka vya Baali. ⁴ Ye waendza Mlungu wa ise na achiphiya sawa na amurize wala kayalunga mahendo ga atu a Iziraeli a vurini. ⁵ Kpwa hivyo Mwenyezi Mlungu wauimarisha hinyo ufalume wa Jehoshafati. Atu

osi a Juda amrehera Jehoshafati zawadi naye achikala ana mali nyinji na achiishimika sana. ⁶ Moyowe wakala imara katika kulunga njira za Mwenyezi Mlungu. Chisha achiusa mwatu mwa dzulu na nguzo za Ashera hiko Juda.

⁷ Tsona, mwaka wa hahu wa utawalawe, Jehoshafati wahuma vilongozie akafundze shariya za Mwenyezi Mlungu kpwenye midzi ya Juda. Nao kala ni Beni-Haili, Obadiya, Zakariya, Nethaneli na Mikaya. ⁸ Hinyo aphiya phamwenga na Shemaya, Nethania, Zebadia, Asaheli, Shemiramothi, Jehonathani, Adonija, Tobija na Tobu-Adonija ambao kala ni Alawi na alavyadzi-sadaka, Elishama na Jehoram. ⁹ Nao kala ana chitabu cha shariya ya Mwenyezi Mlungu, kala achizunguluka midzi yosi ya Juda kufundza atu.

¹⁰ Falume zosi zirizo zunguluka tsi ya Juda zamuogopha Mwenyezi Mlungu nazo taziyahenda viha na Jehoshafati. ¹¹ Afilisti anjina amrehera Jehoshafati zawadi na feza ya kodi. Aarabu nao piya amrehera maturume elufu sabaa na magana sabaa na ndenje elufu sabaa na magana sabaa. ¹² Ukulu wa Jehoshafati waenjerezeka sana naye achidzenga ngome hiko Juda na midzi ya kuika vitu. ¹³ Naye waika akiba ya vitu vinji sana kpwenye midzi ya Juda, na hiko Jerusalemu kala ana majeshi, masujaa a viha. ¹⁴ Hivi ndivyo arivyoandikishwa kulengana na mbari za ise zao. Kula mbari ya Juda akulu a vikosi vya anajeshi elufu-elufu kala ni: Adina, yekala na masujaa a viha elufu magana mahahu. ¹⁵ Wa phiriwe kala ni Jehohanani, naye kala ni

mcpwulu wa anajeshi elufu magana mairi na mirongo minane. ¹⁶ Yemlungira kala ni Amasiya mwana wa Zikiri, mutu yedzitoleya kumuhumikira Mwenyezi Mlungu, kala ana anajeshi hodari elufu magana mairi.

¹⁷ Kula mbari ya Benjamini akulu a vikosi vya anajeshi kala ni Eliada, sujaa naye kala ana anajeshi elufu magana mairi enye maha na ngao. ¹⁸ Wa phiriwe kala ni Jehozabadi, ariyekala na atu elufu gana mwenga na mirongo minane okala tayari na viha. ¹⁹ Hinya ndio okala kpwenye huduma ya mfalume, kanda na hinyo arioikpwa kpwenye midzi yenye ngome, tsi yosi ya Juda.

18

*Mikaya anaonya mfalume Ahabu
wa Iziraeli
(1 Afalume 22:1–28)*

¹ Phahi Jehoshafati kala ana utajiri munji na kala anaishimika sana. Hiye waandzisha uhusiano na mfalume Ahabu wa Iziraeli kpwa kumloza mwanawe mlume, mwana mchetu wa Ahabu.

² Bada ya muda mure, Jehoshafati watserera wakpwendajambosa Ahabu hiko mudzi wa Samariya. Naye Ahabu wamtsindzira iye na atu okala phamwenga naye, mang'ondzi manji na ng'ombe nyinji sana. Chisha achimchenga-chenga aphiye phamwenga akapigane na atu a Ramothi-Giliadi. ³ Ahabu, mfalume wa Iziraeli achimuuza Jehoshafati mfalume wa Juda, “Dze! Undaphiya nami ko Ramothi-Giliadi?”

Naye achijibu achiamba, “Mino ni dza uwe na atu angu ni dza atuo, naswi hundakala phamwenga nawe vihani.”⁴ Ela Jehoshafati achimuamba mfalume wa Iziraeli, “Kpwandza kauze Mwenyezi Mlungu ushauri.”

⁵ Phahi, mfalume wa Iziraeli wakusanya manabii ambao kala ni kama magana mane, achi-auza, “Niphiye hebu nisiphiye kuupiga viha Ramothi-Giliadi?” Nao amjibu, “Ambuka kpwa kukala Mlungu andautiya mwako mkpwononi uwe mfalume.”

⁶ Ela Jehoshafati achiuza achiamba, “Dze! Phano taphana nabii wanjina wa Mwenyezi Mlungu ambaye hunaweza kumuza ushauri?”

⁷ Naye mfalume wa Iziraeli achimjibu Jehoshafati achimuamba, “Phasere mutu mmwenga, Mikaya mwana wa Imula, ambaye hunaweza kumuza Mwenyezi Mlungu, ela mino namzira, mana kanitabiriya manono ela mai.” Naye Jehoshafati achijibu achiamba, “Hata, mfalume na asiambe hivyo.”⁸ Ndipho mfalume wa Iziraeli achiiha ofisaawe mmwenga achimuamba, “Henda wangbwi umrehe Mikaya mwana wa Imula.”

⁹ Phahi mfalume wa Iziraeli na Jehoshafati mfalume wa Juda kala chila mmwenga akasagarira chihiche cha endzi, kpwenye muhala wa kuwagira mtsere, kpwenye ryango ra Samariya. Kala akavwala mavwazi gao ga chifalume, na nyo manabii osi kala anatabiri mbere zao.

¹⁰ Naye Zedekiya mwana wa Kenaana wadzitengezera pembe za chuma, na

achiamba, “Mwenyezi Mlungu anaamba hivi, ‘Mundaasukuma Aaramu na pembe zizi hadi ndiphoaangamiza.’ ”

¹¹ Nyo manabii anjina osi atabiri dza vivyo, achiamba, “Phiya ukashambuliye mudzi wa Ramothi-Giliadi, undaturya! Mwenyezi Mlungu andautiya mkpwononi mwa mfalume.”

¹² Naye mjumbe ariyekpwendaiha Mikaya, wamuamba Mikaya, “Lola! Manabii anjina analavya unabii kpwa kauli mwenga, kukala ye mfalume andaturya. Sambu uwe nawe kagombe dza aho, na ugombe manono.”

¹³ Ela Mikaya achiamba, “Dza Mwenyezi Mlungu arivyo moyo, neno ndiro gomba Mlungu wangu, ndiro ndirorigomba.”

¹⁴ Mikaya ariphofika, ye mfalume wamuua, “Dze swino huphiye kupiga viha Ramothi-Giliadi hebu husiphiye?” Naye achijibu achiamba, “Ambukani, mkaipige, namwi mundaturya mana andatiywa mwenu mikononi.”

¹⁵ Mfalume achimuamba, “Nikuhende uape kano ngaphi ili uniambire kpweli kpwa dzina ra Mwenyezi Mlungu?”

¹⁶ Naye Mikaya achiamba, “Naona atu osi a Iziraeli akatsamukana dzulu ya myango dza mang’ondzi gasigo na mrisa. Naye Mwenyezi Mlungu achiamba, ‘Atu hinya taana chilongozi. Ariche chila mutu auye kwakpwe kaya na amani.’ ”

¹⁷ Ndipho mfalume wa Iziraeli achimuambira Jehoshafati, “Dze, sikakuambira mino kukala Mikaya kandanitabiriya manono ela mai?”

¹⁸ Mikaya waenderera kugomba achiamba, “Phahi sikira neno ra Mwenyezi Mlungu. Namuona Mwenyezi Mlungu asegere kpwenye chihiche cha endzi, kuno jeshi rosi ra mlunguni riimire mkpwonowe wa kulume na wa kumotso.

¹⁹ Naye Mwenyezi Mlungu achiamba, ‘Ni ani ambaye andamchenga Ahabu mfalume wa Iziraeli, ili aambuke kuphiya Ramothi-Giliadi akaolagbwe kuko?’ Mmwenga achiamba hivi na wanjina anaamba vira.

²⁰ Chisha pepo achidzituluza mbere za Mwenyezi Mlungu achiamba, ‘Mino ndaphiya nikamchenge.’ Mwenyezi Mlungu achimuuza, ‘Chi viphi?’

²¹ Ye pepo achiamba, ‘Ndaphiya nkakale pepo wa handzo miromoni mwa manabiige gosi.’ Naye Mwenyezi Mlungu achimuamba, ‘Haya phiya ukahende hivyo, nawe undafwaulu kumchenga.’ ²² Sambu phahi, uwe mfalume phundza, Mwenyezi Mlungu akatiya pepo wa handzo kanwani mwa hinya manabiigo. Mwenyezi Mlungu akatangaza mai dzuluyo.”

²³ Zedekiya mwana wa Kenaana wamsengerera Mikaya, achimuwanga kofi ra ndzeya na achimuamba, “Ye Roho wa Mwenyezi Mlungu akatulukadze kpwangu ili edze agombe na uwe?”

²⁴ Naye Mikaya achijibu achiamba, “Undamanya yo siku ndiyochimbira, ukadzifwitse chumba cha ndani.”

²⁵ Mfalume wa Iziraeli walavya amuri achi-
 aamba, “Mgbwireni Mikaya mumuuyize kpwa
 Amoni, liwali wa mudzi na kpwa Joashi mwana
 wa mfalume. ²⁶ Mukaambe, ‘Mfalume anaamba
 hivi: Yuyu mutiyeni jela, mumuphe mikahe na
 madzi bahi, hadi ndiphouya salama.’”

²⁷ Mikaya achiamba, “Napho undauya kpwa
 amani, phahi Mwenyezi Mlungu kagombere
 nami.” Na achienjereza achiamba, “Mwimwi
 mosi sikirani!”

Ahabu anafwa hiko Ramothi-Giliadi
(1 Afalume 22:29–30)

²⁸ Phahi mfalume wa Iziraeli na Jehoshafati
 mfalume wa Juda aambuka achiphiya Ramothi-
 Giliadi. ²⁹ Mfalume wa Iziraeli achimuamba
 Jehoshafati, “Mino ndadzihenda avi simi na
 niphye vihani, ela uwe undavwala mavwazigo
 ga chifalume.” Hipo mfalume wa Iziraeli wadz-
 ihenda avi siye, nao achiphiya vihani.

³⁰ Phahi mfalume wa Aramu kala akalagiza
 akulu a magari ga kuvwehwa ni farasi, achi-
 ambira, “Mwimwi msipigane na mutu yeyesi,
 mkpwulu wala mdide, ela mfalume wa Iziraeli
 macheye.” ³¹ Ndipho hinyo akulu a magari ga
 kuvwehwa ni farasi ariphomuona Jehoshafati
 achiamba, “Hiyu ndiye mfalume wa Iziraeli!”
 Kpwa hivyo achimgalukira ili apigane naye.
 Ela Jehoshafati wapiga kululu, naye Mwenyezi
 Mlungu achimtivya. Mlungu wausa akale kure
 naye. ³² Mana nyo akulu a magari ga kuvwehwa
 ni farasi ariphoona kukala siye mfalume wa
 Iziraeli, aricha kumzoresa achiuya.

³³ Ela, mutu mmwenga watonyola uhawe kpwa kubahatisha, achimlatsa mfalume wa Iziraeli kpwenye muungo wa vwazire ra chuma ra kuchinga chifuwa. Hipho Ahabu wamuambira mphiriki wa garire ra kuvwehwa ni farasi, “Galuzza gari uniuse vihani, nkalumizwa.”

³⁴ Na siku iyo viha vyazidi kukala vikali, naye mfalume wa Iziraeli achidzisika-sika ndani ya garire ra kuvwehwa ni farasi, kulola nyo Aaramu hadi dziloni. Dzuwa ririphokala rinatswa achifwa.

19

¹ Jehoshafati mfalume wa Juda wauya salama kpwapkwe kaya Jerusalemu. ² Hipho nabii Jehu mwana wa Hanani, wakpwendakutana naye, achimuuza mfalume Jehoshafati, “Mbona unaterya atu ayi na kuhenda usena na atu amzi-rao Mwenyezi Mlungu? Kpwa kuhenda higo, ukamreyeza Mwenyezi Mlungu. ³ Hata hivyo, ukaonekana wahenda manono kpwa kubananga zo nguzo za Ashera kahi ya yo tsi nawe wadinisa moyoo kumuendza Mwenyezi Mlungu.”

Jehoshafati anaika aamuli akuamula malau

⁴ Jehoshafati wasagala Jerusalemu naye watuluka tsona achianyendekera atu, kula Beerisheba hadi hiko tsi ya myango ya Efuraimu. Wakpwendatiya atu moyo amuuyire Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare ao.

⁵ Watsambula aamuli achiaika chila phenye mudzi urio na ngome himo tsi ya Juda.

⁶ Naye achiaambira ara aamuli, “Zingatiyani

sana munagohenda, kpwa kukala tamuamula kpwa ajili ya mwanadamu ela kpwa ajili ya Mwenyezi Mlungu. Iye a phamwenga namwi munapholavya amulo. ⁷ Sambu phahi, kalani na hofu ya Mwenyezi Mlungu. Dzimanyirireni munagohenda, kpwa mana kpwa Mwenyezi Mlungu, Mlungu wehu takuna kuonera atu, wala kupendeleya, wala kuhongana.”

⁸ Chisha hiko Jerusalemu, Jehoshafati waika Alawi na alavyadzi-sadaka na akulu a mbari za Iziraeli ili alavye uamuli wa Mwenyezi Mlungu na kuamula atu achiokosana. Hinyo ahendera kazi yao hiko Jerusalemu. ⁹ Naye waalagiza achiaambira, “Mundahenda hivyo kpwa hofu ya Mwenyezi Mlungu, kpwa uaminifu na kpwa moyo wosi. ¹⁰ Na chila mtakaphoreherwa lau ni ndugu zenu akalao mwao midzini, rihusuro kumwaga mlatso na kuvundza shariya au amuri au mila, phahi mundaapha mashauri. Hivyo tamundakala na hatiya mbere za Mwenyezi Mlungu, Mlungu akakutsukirirwani, mwimwi na ndugu zenu. Phahi hendani hivyo namwi tamundakala na hatiya. ¹¹ Chisha lolani, hiye Amariya mkpwulu wa alavyadzi-sadaka ndiye ariye dzulu yenu kpwa mambo gosi ga Mwenyezi Mlungu. Naye Zebadia mwana wa Isimaili, chilongozi wa mbari ya Juda, ni wa mambo gosi ga mfalume. Na hinyo Alawi andaahumikira dza maofisaa. Dinani chilume, muhende hivyo naye Mwenyezi Mlungu akale phamwenga na hinyo atu akuhenda haki!”

20

Amoabu na Aamoni anaturywa

¹ Bada ya higo, jeshi ra Amoabu na jeshi ra Aamoni na seemu ya jeshi ra Ameuni akpwedza-pigana na Jehoshafati. ² Bazi ya atu akpwedza achimuambira Jehoshafati, “Likumundi ra majeshi rinakulunga kula Edomu hiko ng’ambo ya bahari. Hivi sambi a hiko Hazazoni-tamari (yani Eni-Gedi).”

³ Jehoshafati waogopha, achiuelekeza usowe kumuendza Mwenyezi Mlungu na achipiga mbiru atu osi a Juda afunge. ⁴ Atu a Juda akusanyika phamwenga ili aendze msada wa Mwenyezi Mlungu. Atuluka kula midzi yosi ya Juda kpwedzaendza Mwenyezi Mlungu.

⁵ Jehoshafati waima mbere ya kusanyiko ra atu a Juda na Jerusalemu, mbere za muhala uriodzengbwa uphya wa nyumba ya Mwenyezi Mlungu. ⁶ Naye achiamba, “Ee Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akare ehu, si ndiwe Mlungu ko mlunguni? Si ndiwe unayetawala falume zosi za mataifa? Mwako mkpwononi muna nguvu na uwezo, usioweza kuzuwiywa ni mutu yeyesi.

⁷ Ee Mlungu wehu, we siwe uriyeazola enyezi a tsi hino mbere za atuo a Iziraeli na uchiapha chivyazi cha msenao Burahimu hata kare na kare? ⁸ Nao asagala himo na achikudzengera phatu phatakatifu ili uabudiwe hipho achiamba, ⁹ ‘Napho hundafikpwa ni janga rorosi, ikale ni viha, au kutiywa adabu, au makongo, au ndzala, hundaima mbere za nyumba hino na mberezo,

mana uwe unaabudiwa ndani ya nyumba hino na hukuririre katika mashaka gehu, uwe undahusikira na uhutivye.’ ¹⁰ Sambu lola, hinya atu a Amoni, Amoabu na a mwango Seiri ambao kuyaruhusu atu a Iziraeli avamie tsi yao ariphola tsi ya Misiri. Hinya arioochwa taayabanangbwa, ¹¹ aredza ahuriphize kpwa kuhuzola kula kpwenye tsi uriyohupha huirisi. ¹² Ee Mlungu wehu, vino hano kundaamula? Kpwa mana swino tahuriweza likumundi hiri ambaro riredza kuhuvamia. Swino tahumanya huendedze, ela matso gehu ganakulola uwe.”

¹³ Alume osi a Juda aima mbere za Mwenyezi Mlungu, phamwenga na ana ao, ahetu aho na ana aho atsanga. ¹⁴ Ndipho Roho wa Mwenyezi Mlungu achimwedzera Jahazieli mwana wa Zakariya, mwana wa Benaya, mwana wa Jeieli, mwana wa Matania, Mlawi wa chivyazi cha Asafu, pho kahi-kahi ya mkpwutano wosi. ¹⁵ Naye achiamba, “Phundzani mwimwi mosi msagalao Juda na Jerusalemu, na uwe mfalume Jehoshafati, Mwenyezi Mlungu anaamba hivi, ‘Msiogophe wala msitishike kpwa ajili ya hiri jeshi kulu kpwa mana viha sivyo vyenu ela ni vya Mlungu. ¹⁶ Muhondo tsererani mkapigane nao. Lolani, nyo andaambuka na njira ya mwango wa Zizi namwi mundaaphahira mwisho wa dete, mbere za weru wa Jerueli. ¹⁷ Tamlondwa kupigana kpwenye viha hivi. Mwimwi atu a Juda na Jerusalemu, dzipangeni

na muhurire, muone vira ambavyo Mwenyezi Mlungu andakutivyani.’ Msiogophe wala msitishike muhondo phiyani mkapigane nao mana Mwenyezi Mlungu a phamwenga namwi.”

¹⁸ Phahi Jehoshafati wazama hadi chitswache chichiguta photsi. Na atu a Juda na Jerusalemu ahenda dza vivyo, osi achimuabudu Mwenyezi Mlungu. ¹⁹ Chisha atu a Lawi kula kpwa mbari za Kohathi na Kora, aima ili amto-gole Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa Iziraeli kpwa raka ra dzulu. ²⁰ Ligundzure alamuka chiti na achituluka kondze kwenye weru wa Tekoa. Aripbokala anatuluka, Jehoshafati waima achiamba, “Atu a Juda na enyezi a Jerusalemu, niphundzani! Aminini Mwenyezi Mlungu namwi mundakalato. Aminini manabiige namwi mundafwaulu.” ²¹ Aripomala kuhenda mashauri na hinyo atu, waika hara ambao andamvwinira Mwenyezi Mlungu na kumtoga kpwa kukala iye ni mnono na ni mtakatifu, kuno anaphiya mbere za rira jeshi achiamba, “Mshukuruni Mwenyezi Mlungu, kpwa mana mendzwaye taisika ta kare na kare.”

²² Nao aripomandza kuimba na kutogola, Mwenyezi Mlungu waika avamizi hiko kpwa atu a Amoni, a Moabu na a mwango wa Seiri, ambao kala akpwezapigana na Juda nao achi-turywa. ²³ Kpwa mana hinyo atu a Amoni na Moabu aagalukira enyezi a mwango wa Seiri achiaangamiza tsetsetse. Nao aripomala kuangamiza hinyo akalao mwango wa Seiri, osi achigalukirana na achiangamizana enye kpwa enye.

²⁴ Jeshi ra Juda ririphofika kwenye mnara wa kurindira hiko jangbwani, akwendalola hiro jeshi kulu. Nao, lola! Osi kala akagbwa photsi ni nyufu taphana ariyetiya. ²⁵ Jehoshafati na atue ariphokpwezahala zewe, akuta unji wa ng'ombe, mali, nguwo na miyo minji ya samani. Ahala miyo minji hata achishindwa ni kuit-sukula. Zewe hizo kala ni nyinji sana hata ichiahala siku tahu kuzitsukula. ²⁶ Iriphofika siku ya ne akusanyika kwenye Dete ra Baraka. Hipo ashukuru na kumtogola Mwenyezi Mlungu, ndiyo mana phatu hipo phaihwa Dete ra Baraka hadi rero.

²⁷ Chisha auya, chila mutu wa Juda na Jerusalemu naye Jehoshafati kala a mbere zao. Auya Jerusalemu na kuhererwa kpwa mana Mwenyezi Mlungu waahenda ahererwe kpwa kuaturya aviha ao. ²⁸ Ainjira Jerusalemu kuno anapiga vinanda, ngephephe na magunda hadi nyumbani mwa Mwenyezi Mlungu.

²⁹ Chisha falume zosi za hizo tsi ziriphosikira kukala Mwenyezi Mlungu akapigana na aviha a Iziraeli, amuogopa Mlungu. ³⁰ Phahi ufalume wa Jehoshafati wahurira kpwa mana Mlunguwe wamupha amani chila uphande.

Jehoshafati anafwa
(1 Afalume 22:41–50)

³¹ Phahi Jehoshafati watawala Juda. Kala ana miaka mirongo mihahu na mitsano ariphoandza kutawala na achitawala kpwa muda wa miaka mirongo miiri na mitsano kula ko Jerusalemu. Nine kala ni Azuba mwana

wa Shilihi. ³² Jehoshafati walunga njira za ise Asa naye kazirichire hata chidide. Wahenda garigo haki mbere za Mwenyezi Mlungu. ³³ Ela kayabananga mwatu mwa dzulu mwa kuabudira, na nyo atu kala taandzangbwe kuika mioyo yao kpwa ye Mlungu wa akare ao.

³⁴ Sambu mahendo ganjina ga Jehoshafati chigosala, hangu mwandzo hadi mwisho, gaandikpwa kpwenye chitabu cha kumbukumbu, cha Jehu mwana wa Hanani na kutiywa kpwenye chitabu cha afalume a Iziraeli.

³⁵ Bada ya hipho Jehoshafati mfalume wa Juda wadziunga na Ahaziya mfalume wa Iziraeli ambaye wahenda mai sana. ³⁶ Wadziunga naye kudzenga meli za kuphiira Tarishishi. Meli hizo zadzengerwa ko Esioni-Geberi. ³⁷ Ndipho Eliezeri mwana wa Dodavahu kula Maresha achilavya unabii chinyume cha Jehoshafati achi-amba, “Kpwa kukala ukagbwirana na mfalume Ahaziya, Mwenyezi Mlungu andabananga vyo urivyotengeza.” Phahi zo meli zavundzika-vudzika na tazi yaweza kuphiya Tarishishi.

21

¹ Phahi, Jehoshafati wafwa, na achizikpwa na akaree kpwenye mudzi wa mkarewe Daudi, na mwanawe Jehoram achitawala badalaye.

Jehoram mfalume wa Juda (2 Afalume 8:16–24)

² Jehoram kala ana nduguze, ana anjina a Jehoshafati ambao ni Azaria, Jehieli, Zakariya, Azariahu, Mikaeli na Shefatia. Hano osi kala ni

ana a Jehoshafati mfalume wa Iziraeli. ³ Ise yao waapha zawadi nyinji za feza, zahabu na vitu vya samani, phamwenga na midzi yenye ngome himo Juda. Ela ufalume wamupha Jehoramu kpwa mana kala ndiye mwanawe mvyere.

⁴ Phahi Jehoramu ariphoandza kutawala na ariphodziimarisha, waaolaga anao osi na piya vilongozi anjina a Iziraeli. ⁵ Jehoramu kala ana miaka mirongo mihahu na miiri ariphoandza kutawala, naye watawala ko Jerusalemu kpwa muda wa miaka minane.

⁶ Jehoramu walunga njira za afalume a Iziraeli dza nyumba ya Ahabu irivyohenda, mana walóla mwana mchetu wa Ahabu. Naye wahenda mai mbere za Mwenyezi Mlungu, ⁷ ela phahi Mwenyezi Mlungu kayalonda kubananga nyumba ya Daudi, kpwa sababu ya chilagane arichokala akachiika naye. Daudi kala waahidiwa kukala andahewa taa phamwenga na chivyaziche hata kare na kare.

⁸ Siku za utawala wa Jehoramu, atu a Edomu arema kutawalwa kula Juda, achitawaza mfalume wao. ⁹ Jehoramu wavuka na akulu a jeshire phamwenga na magari gosi ga kuvwehwa ni farasi. Usiku wakpwendaapiga Aedomu osi ambao kala akamzangira iye phamwenga na akulu a jeshi a magari ga kuvwehwa ni farasi. ¹⁰ Hivyo ndivyo atu a Edomu arivyorema kutawalwa ni Juda hadi rero. Wakati uho-uho atu a mudzi wa Libuna nao piya

arema utawala wa Jehoramu mana wamricha Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa akaree.

¹¹ Kuuya phapho, iye wadzenga mwatu mwa dzulu mwa ibada hiko tsi ya myango ya Juda na achiaakoseza enyezi a Jerusalemu uaminifu na achiahenda aaphuke njira. ¹² Wareherwa baruwa kula kpwa nabii Elija, ichimuamba, “Hivi ndivyo Mwenyezi Mlungu, Mlungu wa sowe Daudi anavyokuamba, ‘Kpwa kukala kukalunga njira za sowe Jehoshafati, wala njira za Asa mfalume wa Juda, ¹³ ela ukalunga njira za afalume a Iziraeli. Atu a Juda na enyezi a Jerusalemu ukaalongoza kuabudu vizuka dza vira Ahabu na nyumbaye arivyohenda. Piya ukaolaga enenu, ana a sowe ambao kala ni atu anono kuriko uwe. ¹⁴ Kpwa kukala ukahenda mai higo Mwenyezi Mlungu andareha mashaka makulu kpwa atuo, anao, acheo na kpwa maliyo yosi. ¹⁵ Na we mwenye, undagbwirwa ni ukongo mui wa mahumbo ambao undazidi chila siku, undalumwa sana hadi mahumbogo gatuluke kondze.’ ”

¹⁶ Ndipho Mwenyezi Mlungu achiafyakatsira Afilisti na Arabu ambao kala ni majirani na Akushi apigane na Jehoramu. ¹⁷ Nao ashambuliya Juda achihala mali yosi ariyoiphaha nyumbani mwa mfalume, phamwenga na anae na ahee. Wasazirwa mwana mmwenga tu mdide, yeihwa Jehoashi.

¹⁸ Bada ya higo kuhendeka, ndipho Mwenyezi Mlungu achimrehera Jehoramu ukongo wa mahumbo usiophola. ¹⁹ Ukongo wa Jehoramu waenderera kuzidi na kufikira mwisho

wa mwaka wa phiri wa ukongowe mahumboge gatuluka na achifwa kpwa maumivu makali. Wala atue taayaasa moho mkpwulu kumupha ishima dza arivyohenderwa akaree.

²⁰ Jehoramu kala ana miaka mirongo mi-hahu na miiri ariphoandza kutawala, naye watawala miaka minane hiko Jerusalemu. Chi-foche tachiyasonones a yeyesi, naye wazikpwa kpwenye Mudzi wa Daudi ela siyo vikurani pha afalume.

22

Ahaziya mfalume wa Juda

(2 Afalume 8:25–29; 9:21–28)

¹ Bada ya chifo cha Jehoramu, enyezi a Jerusalemu amuhenda Ahaziya, mwana mdide wa mfalume atawale badalaye. Ana avyere a mfalume kala akaolagbwa ni vikosi vyokp-wedza phamwenga na Aarabu kuchita kambi. Kpwa hivyo Ahaziya mwana wa mfalume Je-horamu wa Juda achitawala. ² Ahaziya kala ana miaka mirongo miiri na miiri ariphoandza kutawala. Naye watawala kpwa muda wa mwaka mmwenga ko Jerusalemu. Nine kala aihwa Athalia, mdzuku wa Omuri. ³ Hiyu naye walunga njira za nyumba ya Ahabu kpwa mana kala anashauriwa ni nine ahende mai. ⁴ Wahenda garigo mai mbere za Mwenyezi Mlungu dza arivyohenda Ahabu. Ise wa Ahaziya ariphofwa, atu a nyumba ya Ahabu ndio okala ashaurie nao achimuangamiza. ⁵ Ahaziya walunga sana mashauri gao hata achiphiya

